# Mpango wa Dharura wa Familia

## MPANGO WA DHARURA NI NINI?

Mpango wa Dharura ni hati ambayo kila mtu anapaswa kuwa nayo ili kujilinda yeye mwenyewe na familia yake wakati wa dharura, iwe ni moto, ugonjwa, au kukamatwa na maafisa wa ICE (Idara ya Uhamiaji).

Hati hii ina taarifa muhimu kuhusu kila mwanachama wa familia yako.

USIBEBE MPANGO WAKO WA DHARURA KILA WAKATI!

Hakikisha umeweka mahali salama pamoja na nyaraka nyingine muhimu - kama pasipoti yako, maagizo ya dawa za matibabu, na nyaraka nyingine za uhamiaji.

ONYESHA MAHALI ULIPO HIFADHI MPANGO WAKO WA DHARURA KWA MARAFIKI AU NDUGU UNAOWAAMINI PEKEE.

Hakikisha wanajua ulipo, kwa nini ni muhimu, na jinsi ya kupata ikiwa utahitaji.

USIMWEONYESHE WAKALA WA ICE MPANGO WAKO WA DHARURA!

## MTU WA KUWASILIANA NAYE WAKATI WA DHARURA' AU' MTU MZIMA UNAYEMWAMINI" NI NANI'?

Mtu wa kuwasiliana naye wakati wa dharura ni mtu ambaye unaweza kumpigia simu ikiwa jambo lisilo mtarajiwa litakutokea wewe au familia yako. Anaweza kuwa familia, rafiki, au jirani anaye kufahamu wewe na familia yako.

Huyu ni mtu ambaye unaweza kumtegemea kwa msaada wa haraka unapojaribu kutatua hali iliyotokea.

Anaweza kukusaidia kupata huduma, kupeleka kwa daktari, au hata kuwachukua watoto wako shuleni.

Ni jambo nzuru kutoa maelezo ya mtu wako wa dharura mahali pako pakazi na katika shule za watoto wako.

Mtu mzima unayemwamini ni mtu ambaye unamwamini kuwalea watoto wako ikiwa jambo lolote litakutokea.

Mtu huyu anapaswa kuwa wa kuaminika na aweze kuwachukua watoto wako shuleni inapohitajika. Ikiwezekana, inashauriwa kuchagua mtu aliye na Green Card au raia wa Marekani.

## NYARAKA MUHIMU

Hii ni orodha ya nyaraka muhimu ambazo unapaswa kujaza kwa ajili ya familia yako na kuzihifadhi mahali salama. Pia unapaswa kushiriki nakala zake na watu wako wa dharura na watu wazima unaowaamini.

Fomu hizi zinapaswa kujazwa kwa kalamu yenye wino mweusi.

Mpango wa Dharura wa Familia

Hii ni hati yenye taarifa muhimu kuhusu wanachama wote wa familia yako.

Fomu ya Mawasiliano ya Dharura na Ruhusa ya Kuwachukua Watoto Shuleni

Hii ni hati inayoruhusu watu unaowaamini kuwachukua watoto wako kutoka shuleni ikiwa huezi kufanya hivyo mwenyewe. Unapaswa kujaza fomu moja kwa kila mtoto anayesoma shuleni. Fomu hii inapaswa kuwasilishwa kwa shule ya mtoto wako.

Fomu ya Ice 60-001: Kibali cha Faragha cha Kuruhusu Utoaji wa Tarifa kwa Mtu wa Tatu.

Fomu hii inaruhusu mtu mzima unayemwamini kuzungumza na maafisa wa ICE ikiwa umewekwa kizuizini. Anaweza kuwauliza maswali kuhusu kesi yako ili kukusaidia. Fomu hii lazima isainiwe na shahidi ambaye si mwanafamilia wako wala mtu mzima aliyeteuliwa kwenye fomu. Unaweza kupata fomu hii mtandaoni.

AR-11: Fomu ya Kubadilisha Anwani

Fomu hii inajulisha serikali ya Marekani (USCIS) kuhusu anwani yako mpya ikiwa utahama. Ikiwa wewe si raia wa Marekani, unatakiwa kisheria kujulisha anwani yako ndani ya siku 10 baada ya kuhama. Unapaswa kujaza fomu kwa kila mwanachama wa familia yako. Watoto wenye umri wa miaka 14 na zaidi wanapaswa kusaini fomu zao wenyewe. Unaweza kusaini kwa niaba ya watoto walio chini ya miaka 14.

Unaweza kupata fomu hii mtandaoni.

## Mapendekezo Mingine

WEKA PROGRAMU YA READYNOW KWENYE SIMU YAKO

Tafuta "ReadyNow" kwenye (App Store) au (Google Play Store) na ufuate maelekezo ya kuiweka. Programu hii hukuwezesha kubonyeza kitufe (button) kinachotuma ujumbe kwa watu wako wa dharura ikiwa utakamatwa na ICE.

KARIRI NAMBA MUHIMU ZA SIMU

Kariri namba za wanafamilia wako na watu wako wa dharura.

BEBA NYARAKA MUHIMU

Watu wote ambao si raia wa Marekani wanatakiwa kubeba ushahidi wa kibali yao ya uhamiaji. Ikiwa una Green Card, lazima uibebe. Wengine wanapaswa kubeba hati nyingine inayothibitisha hadhi yao, kama vile fomu ya I-94. Ikiwa una ombi yanayosubiri kushughulikiwa na USCIS, unapaswa kubeba nakala ya stakabadhi ya kupokea ombi hilo.

Ikiwa huna mojawapo ya nyaraka hizi, beba kitambulisho cha jimbo, kitambulisho cha manispaa,au leseni ya kuendesha gari. Usibebe nyaraka za uwongo.

Muulize wakili wako wa uhamiaji akuthibitishie nyaraka unazopaswa kubeba

FAHAMU HAKI ZAKO

Kila mtu ana haki bila kujali hadhi yake ya uhamiaji. Hakikisha kila mtu katika familia yako anaelewa haki zake.

Unaweza kutazama video kwenye chaneli ya YouTube ya Hello Neighbor ili kujifinza kuhusu haki zako kwa lugha za Kiarabu, Kiengereza, Dari, Pashto, Kihispania, Kifaransa, Kisomali, na Kiswahili.

Unaweza kubeba Cadi Nyekundu (Red Card). Kadi hizi huwekwa kwenye pochina zinaorodhesha haki zako wakati wa mawasilianona vyombo vya sheria , ikiwemo ICE. Kadi nyekundu za bure zinapatikana katika lugha 59 kupitia tovuti ya Immigran Legal Resource Center (ILRC).

WASILISHA MAOMBI YA ULEZI WA DHARURA

Tunapendekeza ukutane na wakili wa masuala ya familia ili kuwasilisha nyaraka za ulezi wa dharura. Hii ni hati rasmi inayobainisha ni nani unayemtaka awatunze watoto wako ikiwa jambo lolote lisolotarajiwa litakutokea. Mchakato unaweza kutofautiana kulingana na jimbo au eneo unaloishi.

Ikiwa uko Pittsburgh na unaona au kushuhudia shughuli za ICE, unaweza kuripoti kwa Casa San Jose kwa: 412-736-7167.

**MPANGO WA DHARURA WA FAMILIA YANGU**

| |
|---|
| Majina, Tarehe za Kuzaliwa, na Nchi za Kuzaliwa za watu wote wazima walioko nyumbani: |
| Nchi za Asili za watu wazima wote walioko nyumbani |
| Majina, Tarehe za Kuzaliwa, na Nchi za Kuzaliwa za watoto wote walioko nyumbani |
| Nchi za Asili za watoto wote nyumbani |
| Anwani: |
| Manispaa: |

| |
|---|
| Nambari ya simu ya wanajamii wote: |
| Lugha Inayopendelewa: |
| Lugha nyingine: |
| A-Numbers ya wanakikundi wote: |
| Nambari ya Mwasiliano wa Dharura #1:<br><br>Jina:<br><br>Nambari ya Simu: |
| Nambari ya Mwasiliano wa Dharura #2:<br><br>Jina:<br><br>Nambari ya Simu: |
| Mtu mzima anayeelezwa kwa kuaminika kwa ajili ya kulea watoto wangu<br><br>Jina:<br><br>Nambari ya Simu: |
| Majina Muhimu ya Familia na Nambari za Simu (jumuisha nambari za Whatsapp za mawasiliano ya kimataifa) -- hawa ndicho watu ungependa kuwajulisha wakati wa dharura. |

| |
|---|
| Ofisi ya Daktari Wangu: |
| Jina la Daktari Wangu: |
| Nambari ya Simu ya Daktari Wangu: |
| Hali zangu au upasuaji: |
| Ninachukua dawa hizi na kipimo chao: |
| Mzio au mahitaji yangu ya chakula: |
| Kazi ninayofanya: |
| Jina la Mkuu Wangu: |
| Nambari ya Simu ya Msimamizi Wangu: |
| Wanyama wa Nyumbani (jina, aina ya mnyama): |

## Taarifa za Watoto

| |
|---|
| Watu Wakubwa Katika Kaya: |

| |
|---|
| MTOTO<br><br>Jina:<br><br>Tarehe ya Kuzaliwa:<br><br>Shule:<br><br>Hali za Matibabu:<br><br>Dawa na Dozi:<br><br>Mzio:<br><br>Miadi ya Tiba Iliyokuja: |
| MTOTO<br><br>Jina:<br><br>Tarehe ya Kuzaliwa:<br><br>Shule:<br><br>Hali za Matibabu:<br><br>Dawa na Dozi:<br><br>Mzio:<br><br>Miadi ya Tiba Iliyokuja: |

**Taarifa za Watoto**

| |
|---|
| Watu Wakubwa Katika Kaya: |

| |
|---|
| MTOTO<br><br>Jina:<br><br>Tarehe ya Kuzaliwa:<br><br>Shule:<br><br>Hali za Matibabu:<br><br>Dawa na Dozi:<br><br>Mzio:<br><br>Miadi ya Tiba Iliyokuja: |
| MTOTO<br><br>Jina:<br><br>Tarehe ya Kuzaliwa:<br><br>Shule:<br><br>Hali za Matibabu:<br><br>Dawa na Dozi:<br><br>Mzio:<br><br>Miadi ya Tiba Iliyokuja: |

# Fomu ya Mwasiliano wa Dharura na Kuinuliwa Shule kwa Idhini

Taarifa za Mwanafunzi

| |
|---|
| Jina Kamili: |
| Tarehe ya Kuzaliwa: |
| Daraja: |

Taarifa ya Mzazi/Mlezi

| |
|---|
| Jina: |
| Uhusiano na mwanafunzi: |
| Nambari ya Simu: |
| Anwani: |
| Barua pepe: |

Watu wenyevyo wametolewa ruhusa kuchukua mwanafunzi uliotajwa hapo juu kutoka shule na kufanya maamuzi endapo nisingepatikana.

| |
|---|
| Jina:<br><br>Uhusiano na mwanafunzi:<br><br>Nambari ya Simu: |
| Jina:<br><br>Uhusiano na mwanafunzi:<br><br>Nambari ya Simu: |

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: ____________________________________________Tarehe: _________